# Jedwali la Kazi la Kubuni Shughuli

Jedwali hili la kazi ni mwongozo muhimu wa kubuni shughuli za mradi wako. Kwanza, zipe kipaumbele shughuli unazotaka kutekeleza. Kisha jedwali hili la kazi litakusaidia kutambua vipengele vya "nani?, nini?, wapi?, lini? na kwa nini?" kwa kila shughuli na kuanza mchakato wa kuchanganua matatizo, masuala au hatari zinazoweza kujitokeza ambazo huenda ukakumbana nazo unapotekeleza mpango wako. Moduli ya Kutekeleza itagusia hatari zinazoweza kujitokeza na mbinu za kudhibiti hatari kwa kina.

| JEDWALI LA KAZI LA KUBUNI SHUGHULI |
|---|
| **NINI: Jina la Mradi, Jina la Shughuli na Lengo Linalohusiana na Mradi** |
| **KWA NINI: Shughuli itachangiaje katika kutimiza lengo husika?** |
| **NANI: Washiriki/Wanufaishwa Wanaolengwa (weka maelezo mengi kadri iwezekanavyo, idadi ya washiriki, kutoka nchi gani, n.k.)** |
| **VIPI:**<br>**Mbinu:**<br><br>Nyenzo Zinazohitajika: |
| **WAPI:** |
| **LINI: Shughuli itafanyika wakati gani, kuna vipindi vya muda vilivyowekwa ambavyo lazima uvizingatie (k.m. sikukuu tofauti za kitaifa na kidini, nyakati za siku, n.k)** |

| MASUALA YA KUZINGATIA | |
|---|---|
| | |
| **HATARI ZINAZOWEZA KUJITOKEZA** | |
| Kipengele cha Hatari | Mbinu ya Udhibiti |
| | |

## Hati ya Marejeleo: Mifano ya Miradi ya P/CVE

Shirika la Hedayah na Search for Common Ground yalitunga orodha ya shughuli mbalimbali za miradi ya P/CVE kwenye mtaala wao wa mafunzo: Countering Violent Extremism: An Introductory Guide to Concepts, Programming, and Best Practices. Mchakato wa kubuni shughuli za mradi wa P/CVE unapaswa kutokana na muktadha wako, ukadiriaji wa shughuli za VE na mgogoro, nadharia ya mpango na uwezo wa shirika lako. Hata hivyo, hii inatumika kama orodha ya mfano ya aina mbalimbali za shughuli za P/CVE za kukupa mawazo kuhusu kitu ambacho kimefanywa na mashirika mengine katika sekta hii.

## SEHEMU ZA SHUGHULI ZA MIRADI YA P/CVE

### ULINZI WA JUMLA

- Kuanzisha mazungumzo kati ya tamaduni mbalimbali ili kukuza ustahimilivu kati ya tamaduni hizo na kutambua sehemu za kushirikiana katika jamii kwenye sehemu ambazo migawanyiko katika jamii ni visababishi vya shughuli za makundi yenye itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu.
- Kuwapa mafunzo wafanyakazi wa vyombo vya habari kuhusu jinsi ya kutangaza kitaalamu matukio ya vurugu na ya kuzua wasiwasi kwa njia ambazo zinazuia kuleta mihemko, kushutumu jamii mahususi au kuongeza migawanyiko.
- Kukuza ujuzi wa kusuluhisha mgogoro kwa viongozi wa jamii ili kushughulikia hali za kuleta wasiwasi katika eneo, kujenga maelewano kuhusu matatizo ya pamoja na kuanzisha juhudi za pamoja ili kuyasuluhisha katika sehemu ambazo migogoro ya jamii ni visababishi vya shughuli za makundi yenye itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu.
- Kufanya utafiti kuhusu hatari inayoweza kusababishwa na shughuli za makundi yenye itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu katika muktadha mahususi na sehemu na miktadha mahususi ambayo iko katika hatari ya kuathiriwa na inayohitaji zaidi mpango wa kukabiliana na shughuli za makundi yenye itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu.
- Kusaidia viongozi wa kidini kushughulikia suala la fafanuzi za kiitikadi kali za dini na makundi yenye itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu kwa kutumia mbinu stahimilivu za dhana za kawaida za kidini katika sehemu ambazo dini hutumiwa kushawishi watu kujiunga na makundi ya dhana za itikadi zinazohimiza matendo ya vurugu.
- Kuboresha mbinu za kukabiliana na shughuli za makundi yenye itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu katika viwango vya serikali, usalama, asasi za kiraia na eneo kupitia kutoa usaidizi na kukuza uwezo.
- Kuboresha uwezo wa kutafuta haki, usaidizi wa kisheria na ufanisi wa mifumo ya haki katika jamii wakati masuala haya ni visababishi vya shughuli za makundi yenye itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu.
- Kukuza uthabiti katika vijana kupitia nyenzo za elimu ambazo zinazungumzia dhuluma na utambulisho na kukuza uwezo wa kufikiria kwa undani na maarifa ya ufahamu wa teknolojia wakati masuala haya yamebainishwa kwamba husababisha uwezekano wa kushawishika kukubali dhana za itikadi kali.
- Kuhamasisha na kukuza uwezo wa kushughulikia shughuli za makundi yenye itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu katika sekta ya elimu kupitia kushirikiana na vijana, walimu, maprofesa na taasisi.
- Kukuza mahusiano mazuri ya uaminifu na heshima kati ya polisi na jamii wakati mahusiano mabaya yamebainishwa kuwa kisababishi cha shughuli za makundi yenye itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu.

## ULINZI MAALUM

- Kukuza mshikamano wa kijamii kupitia ujumuishwaji na kushiriki kwa makundi ya kijamii yaliyotengwa wakati makundi haya yamebainishwa kuwa yanaweza kushawishika kukubali dhana za itikadi kali kutokana na sababu hizi.
- Kukuza elimu muhimu ya teknolojia na vyombo vya habari kwa vijana waliobalehe na watu wenye umri mdogo wanaoweza kushawishika, kuwa thabiti na kutokubali dhana za itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu kuhusu maisha, utambulisho, dini na shughuli za kijamii au za kisiasa.
- Kukuza uthabiti wa watu wanaoweza kushawishika kwa kuwasaidia kukuza ujuzi wa kuondoa msongo wa mawazo, kudhibiti hisia zao, kutoshawishika kukubali dhana za itikadi kali na ushawishi wa wenzao na kusuluhisha migogoro kwa kutumia njia ya amani.
- Kutumia shughuli za spoti, sanaa na shughuli nyingine ili kukuza mahusiano kati ya vijana wanaoweza kushawishika na kutoa vipindi vya mafunzo ili kuwapa mitazamo halisi kuhusu masuala ya kijamii na ya kisiasa.
- Kusaidia vijana wanaoweza kushawishika kuelewa vyanzo, dalili na matokeo ya kushawishika na dhana za itikadi kali na jinsi watu wanavyoweza kujiepusha na mtindo huo wa maisha kupitia mfululizo wa ushahidi wa video kutoka kwa watu waliokuwa wanachama wa zamani wa makundi yenye itikadi kali.
- Kuunda mtandao wa vijana na wakufunzi wa vijana ambao wako tayari kuzuia shughuli za kushawishi watu kukubali dhana itikadi kali na kuwa vielelezo kwa vijana wanaoweza kushawishika kukubali dhana za itikadi zinazohimiza matendo ya vurugu.
- Kushirikisha vielelezo wa eneo kutoka kwenye jamii zinazoweza kushawishika au ambao walikuwa wanachama wa zamani wa makundi yenye itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu ili kuzuia kutokea kwa migawanyiko mikali na ushawishi wa wtu kukubali dhana za itikadi kali kati ya jamii kwa kuhimiza kufanywa kwa mazungumzo kati ya raia wanaoweza kushawishika na kwa kupanga shughuli za uzuiaji.
- Kuwapa mafunzo akina baba na akina mama waliofungwa gerezani ambao wanaonyesha mitazamo ya watu wenye itikadi kali (ambao kwa hivyo wanaweza kuwafunza watoto wao mitazamo hiyo) ya kukubali mitazamo mizuri pamoja na madarasa ya uzazi ili kuzuia wasiwafunze watoto wao dhana za itikadi kali.

## UZUIAJI WA MAPEMA/KUBADILISHA MTAZAMO

- Kuweka nambari ya simu ya dharura ya kupigwa na wazazi na wanajamii wengine ambao wanashuku mtu ambaye anaonekana kuwa ameshawishika na dhana za itikadi kali.
- Kuongeza kiwango cha uhamasishaji wa polisi na maofisa wa magereza katika kutambua mapema dalili za mtu aliyeshawishika na dhana za itikadi kali kwa kuimarisha ujuzi wao wa utambuzi na ukadiriaji.
- Kurekodi na kushiriki ushuhuda wa kubadilisha maisha wa watu waliohusika au walioumizwa na shughuli za makundi yenye itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu ili kufichua uvumi wa uongo wa makundi yenye dhana za itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu ambao hadhira lengwa inapokea.
- Kubuni mbinu ya kutoa mwongozo na usaidizi kwa walimu wanaokumbana na matukio ya wanafunzo kushawishi wengine kukubali dhana za itikadi kali madarasani.
- Kushughulikia mapema hali za kushawishika na dhana za itikadi kali kwa kushirikiana kwa pamoja na wafanyakazi wa umma, wafanyakazi wa vijana, madaktari wa magonjwa ya akili na polisi.
- Kulenga watu wanaotafuta ujumbe wa dhana za itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu mtandaoni na kuwaelekeza kwenye video za YouTube zilizoratibiwa ambazo zinafichua mada za kikundi hicho za kushawishi watu kujiunga nacho.

## KUJITENGA NA/AU KUACHANA NA DHANA ZA ITIKADI KALI

- Kutekeleza mkakati wa kusaidia watu walioshawishika na dhana za itikadi kali kujiondoa katika makundi yenye dhana za itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu kwa kuimarisha mahusiano katika familia na kuwasaidia kupata kazi na makundi mazuri ya kijamii.
- Kutoa huduma za ushauri wa mtu binafsi kwa watu waliojiondoa katika makundi yenye dhana za itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu na kufichua njia ambazo zilitumiwa na makundi yenye dhana za itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu ili kuwashawishi na makosa ya uhalifu waliofanya.
- Kutangaza vipindi vya redio katika maeneo ambapo makundi yenye dhana za itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu hutekeleza shughuli zake ili kuyahimiza yaache matendo yake ya vurugu na kuyafahamisha kuhusu mipango ya serikali inayopatikana ya kuyasaidia kukomesha shughuli zake.

- Kubuni mpango wa watu waliofungwa gerezani ambao wameshawishika na dhana za itikadi kali au wamefungwa kwa sababu ya makosa ya shughuli za makundi yenye itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu, ambao unawaruhusu kutathmini upya mitazamo yao ya maisha na kuunda mahusiano bora na watu waliowachukulia kama adui.
- Kusaidia wanachama wa zamani wa makundi yenye itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu kushiriki hali zao za kujiondoa katika kundi yenye itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu na kuwatia moyo wengine wafanye hivyo.
- Kutoa usaidizi na mwongozo kwa makundi yenye dhana za itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu na vijana wanaoshikilia dhana za itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu ambao wako tayari kuondoka katika eneo na mazingira yaliyoshawishika na dhana za itikadi kali.

## UREKEBISHAJI WA TABIA

- Kuhoji wahalifu wa makosa ya shughuli za makundi yenye itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu walio gerezani kuhusiana na dhana inayowatia motisha na mikakati waliyotumia kuhalalisha makosa yao na kuwapa ushauri wa kabla ya kuruhusiwa kuondoka gerezani wa kuwasaidia wachambue misingi hii na kutafuta njia nyingine bora badala yake.
- Kuwapa ushauri wafungwa walioshtakiwa kwa/au kufungwa kwa sababu ya makosa ya kigaidi pamoja na wafungwa wanaoweza kushawishika na dhana za itikadi kali, ili kuwasaidia wasuluhishe matatizo na migogoro kwa kuchagua mtindo wa maisha usio wa kihalifu, ikijumuisha mtandao wa wafungwa wa nje ya gereza na kuwasaidia kukabiliana na changamoto watakazokumbana nazo baada ya kuruhusiwa kuondoka gerezani.
- Kuwapa wapiganaji waliokwenda kupigana nje ya nchi ambao wamerejea mbinu za kusuluhisha mgogoro na usaidizi wa kukabiliana na hali zinazosumbua akili.

## KUJUMUISHWA TENA KATIKA JAMII

- Kusaidia wanachama wa zamani wa makundi yenye itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu kurejea tena katika jamii kwa kuwahimiza kushiriki katika shughuli za amani za kisiasa na kutenda matendo mazuri katika jamii.
- Kushirikiana na jamii ili kuzuia hali ya kushutumiwa kwa watoto walioathiriwa katika jamii za wapiganaji waliokwenda kupigana nje ya nchi au familia zinazorejelea, hali ambayo inaweza kusababisha kutengwa au hata kuwatia moyo wa kujiunga na jamaa zao walio kwenye makundi yenye itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu.
- Kusaidia wanachama wa zamani wa makundi yenye itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu wanaorejea ili warejelee hali yao katika jamii kwa kuwasaidia kuwa wanaharakati wa kupinga shughuli za kushawishika na dhana za itikadi kali na kujiunga na makundi yenye itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu.

**Sifa**: Hati hii ya marejeleo inatumia mifano ya miradi ya kukabiliana shughuli za makundi yenye dhana za itikadi kali zinazohimiza matendo ya vurugu kutoka kwenye nyenzo ya Impact Europe's Countering Violent Extremism Database Search katika http://www.impact.itti.com.pl/index#/inspire/search, Radicalization Awareness Network's (RAN) Collection katika https://ec.europa.eu/home-affairs/what-we-do/networks/radicalisation_awareness_network/ran-best-practices/ran-search_en na kutoka kwenye nyenzo ya The Future of Countering Violent Extremism: An Analysis of Current Programming in Jordan iliyoandikwa na Patrick Stahl na Julia Wilton (Center for Global Affairs at New York University).